NATNETS
National Insecticide Treated Nets Programme

# NATnets news

Toleo Na. 10 Februari-Aprili 2009

## Balozi wa Malaria wa Afrika Ahudhuria Maadhimisho ya Siku ya Malaria Duniani Mkoani Mtwara




*Yvonne Chakachaka*

Balozi wa malaria na mwanamuziki maarufu barani Afrika, Bi. Yvonne Chaka Chaka alihudhuria maadhimisho ya Siku ya Malaria Duniani nchini Tanzania, akiambatana na viongozi wa kitaifa na serikali za mitaa, pamoja na wanajamii. Mwaka huu sherehe za maadhimisho ya Siku ya Malaria Duniani zilifanyika kitaifa mkoani Mtwara tarehe 25 Aprili. Kauli mbiu ya Siku ya Malaria Duniani kwa mwaka 2009 ni *"Tokomeza Malaria"*. Kauli mbiu hii ilitumika kukumbusha msimamo wa kupunguza nusu ya maambukizo na vifo vitokanavyo na ugonjwa wa malaria barani Afrika ifikapo mwaka 2010 uliowekwa mnamo tarehe 25 Aprili 2000 na Viongozi wa Nchi za Afrika huko jijini Aduja, Nigeria.

*(Inaendelea Uk. 4)*

## Ndani ya toleo hili:

**Ukurasa 2**
- Tahariri
- Serikali ya Uswizi yafadhili kitengo cha ITN

**Ukurasa 3**
- Mikakati ya Kuwalinda Walio Hatarini na Malaria …

**Ukurasa 4**
- Mganga Mkuu wa Mpanda Atudokeza Mafanikio ya Kampeni
- Mbinu za Kutatua Changamoto za Matumizi ya Vyandarua Vyenye Dawa

## Zaidi ya Walengwa Milioni 4.3 Wafaidika na Hati Punguzo

Mpango wa Taifa wa Hati Punguzo unasongambele katika kuwakinga wajawazito na watoto na ugonjwa wa malaria. Hadi kufikia Januari 2009, zaidi ya wajawazito na watoto milioni 4.3 wametumia Hati Punguzo kununua vyandarua vyenye dawa ya kudumu. Hii inonyesha ongezeko la zaidi ya asilimia 8, ukilinganisha na idadi ya Hati Punguzo za Wajawazito na Watoto zilizotumika hadi kufikia mwisho wa mwezi Septemba 2008.

Kupitia mpango huu, kila mjamzito na kila mtoto mwenye umri wa chini ya 9 anayehudhuria kliniki anajipatia Hati Punguzo yenye thamani ya shilingi za Kitanzania 3,250/-, ambayo kuweza kutumika kununua chandarua chenye dawa kinachoambatana na dawa ya NGAO iliyoboreshwa.

Pamoja na hayo, kuna mipango mbalimbali ya kupanua mpango huu kupitia Mkakati wa Keep-up utakaowawezesha walengwa kununua vyandarua vyenye dawa ya kudumu kwa kutumia Hati Punguzo mpya, ambapo walengwa watalipa Tsh 500/=. Utekelezaji wa mkakati wa Keep-up unategemewa kuanza baadae mwaka huu.




## Waziri wa Afya Azindua Kampeni ya Usambazaji wa Vyandarua

Tarehe mbili mwezi wa tatu mwaka huu, Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Profesa David Mwakyusa, alizindua rasmi kampeni ya usambazaji wa vyandarua bila malipo kwa watoto wote wenye umri chini ya miaka mitano huko Mkoani Mbeya wakati wa mkutano wa mwaka wa wahudumu wa afya wa wilaya na mikoa.

Uzinduzi huu umekuja baada ya mafanikio yaliyoonekana kupitia kampeni ya majaribio iliyofanyika wilayani Mpanda mkoani Rukwa hapo Septemba 2008.

Hatua za kuifikisha kampeni hii nchi nzima

*(Inaendelea Uk. 2)*




*Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Prof. David Mwakyusa akitoa chandarua chenye dawa ya kudumu kwa muda mrefu kwa mama mwenye mtoto wa chini ya miaka mitano wakati wa uzinduzi wa kampeni mkoani Mbeya.*

# Tahariri

Baada ya kimya cha muda mfupi, tunayo furaha kukuletea toleo la kumi la *Natnets News*. Tunawashukuru wasomaji wetu wote waliotutumia maoni na maswali mbalimbali yanayohusiana na jarida hili hasa pale uchapishaji uliposimama. Tunatoa shukrani zetu za dhati kwa ushirikiano wenu.

Katika toleo hili, tunaangalia kampeni ya usambazaji wa vyandarua kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano iliyozinduliwa hivi karibuni mkoani Mbeya na Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, wakati wa mkutano wa mwaka wa wahudumu wa afya wa wilaya na mikoa. Inakadiriwa kuwa zaidi ya watoto milioni 7.2 wenye umri chini ya miaka mitano wa Tanzania bara watafaidika na kampeni hii, wakati wanajamii wote watafaidika na zoezi la uwekaji NGAO iliyoboreshwa kwenye vyandarua vyote vya zamani. Haya yote yamewezeshwa na Mfuko wa Fedha wa Dunia wa Kupambana na Ukimwi, Kifua kikuu na Malaria; Benki ya Dunia, Mfuko wa Kupambana na Malaria wa Rais wa Marekani, Malaria No Moro, na Shirika la Maendeleo na Ushirikiano la Uswizi.

Pamoja na hayo, tunawakumbusha wasomaji wetu kuhusu mikakati mbalimbali ya kukuza matumizi ya vyandarua vyenye dawa hasa kwa makundi yaliyo hatarini zaidi na ugonjwa wa malaria. Mikakati hii ni pamoja na Hati Punguzo ya Wajawazito, Hati Punguzo ya Watoto, Mkakati wa Keep-up na Mradi wa Kuelimisha na Kubadili Tabia ya Jamii dhidi ya Malaria Tanzania. Kumbusho hili limekuja wakati muafaka, ambapo tunajitayarisha na maadhimisho ya Siku ya Malaria Duniani hapo tarehe 25 April. Siku hii inaturudisha mwaka 2000, ambapo marais na viongozi wa nchi za Afrika walitia saini makubaliano ya kupunguza zaidi ya nusu ya vifo vinavyotokana na malaria mnamo 2010.

Toleo hili limedhaminiwa na Population Services Internationl(PSI-Tanzania) kupitia Kitengo kinachoratibu maswala ya vyandarua vyenye dawa cha Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria. Tunatoa shukrani zetu za dhati kwa ushirikiano na udhamini.

**NATnets News imetolewa na**
ITN Cell
Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria
S. L. P. 3430
Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2124 977
Nukushi: +255 22 2124 976
Barua-pepe: info@natnets.org

**Imeandaliwa na**
MediaNet Limited
S. L. P. 8608
Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2760 288
Barua-pepe: info@medianettz.com

## Waziri wa Afya Azindua Kampeni ya Usambazaji wa Vyandarua

*(Inatoka Uk. 1)*

zinategemewa kuanzia mkoani Mtwara na Lindi. Katika utekelezaji wa kampeni hii, shughuli kuu ni kusajili watoto wote wenye umri chini ya miaka mitano, zoezi hili linafanyika kwa ushirikiano na Serikali za Mitaa. Shughuli nyingine ni pamoja na kutoa mafunzo kwa wadau wakuu katika ngazi ya wilaya na vijiji, kusambaza vyandarua kwa walengwa, kuweka NGAO iliyoboreshwa kwenye vyandarua vya zamani kwa wanajamii wote, uhamasishaji wa wanajamii kushiriki katika kampeni na ufuatiliaji na tathmini ya zoezi zima.

Kampeni hii itakayotekelezwa Tanzania Bara inategemea kusambaza kadiri ya vyandarua milioni 7.2 kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano na kuweka NGAO iliyoboreshwa kwenye vyandarua vya zamani milioni 6.5 vinavyomilikiwa na wanajamii.

Tafiti mbalimbali zimeonyesha kuwa, matumizi ya vyandarua vyenye dawa yanapunguza vifo vya watoto wachanga kwa asilimia 30 na ugonjwa wa upungufu wa damu kwa wajawazito kwa asilimia 60. Hivyo, kampeni hii inategemewa kupunguza kwa kiasi kikubwa vifo vinavyohusiana na ugonjwa wa malaria kwa watoto na makundi mengine yaliyo hatarini.



*Baadhi ya kinamama waliohudhuria sherehe za uzinduzi Mbeya*

Wadau wakuu katika utekelezaji wa kampeni hii ni pamoja na Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria, mratibu mkuu; World Vision Tanzania, wanaotoa mafunzo kwa wadau wakuu katika ngazi ya wilaya; Mennonite Economic Development Associates (MEDA), hushughulikia usambazaji wa vyandarua; Population Services International (PSI-Tanzania), wanaoshughulika na kampeni za kubadili tabia na uhamasishaji wa jamii; Campaign International, wanaushughulika na kusajili walengwa; na Ifakara Health Institute wanaoshughulika na ufuatiliaji na tathmini.

Kampeni hii inafadhiliwa na Mfuko wa Fedha wa Dunia wa Kupambana na Ukimwi, Kifua kikuu na Malaria; Benki ya Dunia, Mfuko wa Kupambana na Malaria wa Rais wa Marekani, Malaria No More, na Shirika la Maendeleo na Ushirikiano la Uswizi.

Wakati wa uzinduzi wa kampeni hii mkoani Mbeya, Waziri wa Afya alidokeza kuwa kampeni ya usambazaji wa vyandarua vyenye dawa itafuatiwa na *"Kampeni ya Vyandarua kila Sehemu ya Malazi"* ambapo vyandarua vyenye dawa ya kudumu milioni 14 vitatolewa kwa kila familia. Kampeni hii itawezesha kila kaya kumiliki kadiri ya vyandarua 2-3.

## Serikali ya Uswizi Yafadhili Kitengo cha ITN

Serikali ya Uswizi imeendeleza ushirikiano wake wa dhati baada ya kutia saini mkataba wa makubaliano na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania. Kupitia mkabata huu Tanzania itafaidika na ruzuku ya shilingi za kitanzania bilioni 2,714,600,000 kwa muda wa miaka mitatu, kuanzia mwaka 2008-2011. Ruzuku hii itategemewa kuwezesha urabitu wa Mpango wa Taifa wa Vyandarua Vyenya Dawa (NATNETS) kupitia Kitengo kinachoratibu maswala ya vyandarua vyenye dawa (ITN Cell) cha Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria.

Makubaliano haya yalifanyika tarehe 17 Desemba 2008, ambapo Adrian Schlaepfer, Balozi wa Uswizi nchini Tanzania na Mh. Ramandhan Khijjah, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Uchumi kwa niaba ya serikali za nchi zao waliidhinisha ushirikiano wa Serikali ya Uswizi katika kuinua sekta ya afya Tanzania.

Msaada huu unatokana na utambuzi wa kazi kubwa inayofanywa na kitengo kinachoratibu maswala ya vyandarua vyenye dawa katika kurabitu shughuli mbalimbali za Mpango wa Taifa wa Vyandarua Vyenya Dawa ikiwa ni pamoja na usambazaji wa vyandarua vyenye dawa na uwekaji wa NGAO ya kudumu kwenye vyandarua vya zamani, na usambazaji wa Hati Punguzo zinazoyawezesha makundi yaliyo hatarini (wajawazito na watoto) kununua vyandarua vyenye dawa kwa bei nafuu.

> Dhumuni kuu ni kuchangia juhudi za kupunguza vifo vitokanavyo na malaria hasa kwa makundi yaliyo hatarini

Serikali ya Uswizi pia inatambua umuhimu wa kufikia adhimio la Abuja la kupunguza vifo vitokanavyo na malaria ifikapo 2010, pamoja na kufikia Malengo ya Milenia hasa kwa wajawazito na watoto walio chini ya umri wa miaka mitano.

Hivyo basi, dhumuni kuu la ruzuku hii ni kuchangia katika kupunguza vifo vitokanavyo na malaria hasa kwa makundi yaliyo hatarini zaidi na ugonjwa huu. Lengo la kitaifa ni kuhakikisha kuwa mnamo mwaka 2011, asilimia 80 ya wajawazito na watoto wanajikinga na ugonjwa wa malaria kutipia matumizi endelevu ya vyandarua vyenye dawa.

# *Mikakati ya Kuwalinda Walio Hatarini na Malaria ...*

*Mpango wa Taifa wa Hati Punguzo ni mkakati wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na wadau wake, uliojikita katika jitihada za kupunguza vifo vitokanavyo na ugonjwa wa malaria kwa kadiri ya asilimia 80 ifikapo mwaka 2013. Lengo kuu la mpango huu ni kuyalinda makundi yaliyo hatarini zaidi na maambukizi ya malaria (yaani wajawazito na watoto walio chini ya miaka mitano) kwa kuwawezesha kupata vyandarua vyenye dawa kwa bei nafuu zaidi. Lengo hili linatekelezwa kupitia mikakati mbalimbali kama vile Hati Punguzo ya Wajawazito, Hati Punguzo ya Watoto, Kampeni ya Kitaifa ya Kusambaza Vyandarua Vyenye Dawa na Mkakati wa Keep up. Mikakati yote hii inalenga kuongeza upatikanaji, uwezo wa kumiliki na matumizi ya vyandarua vyenye dawa kwa makundi yaliyo hatarini zaidi na ugonjwa huu. Mikakati hii ina uhusiano wa karibu na hivyo basi husaidiana katika jitihata za kufikia malengo ya Mpango wa Taifa wa Hati Punguzo. Katika sehemu hii tunaangalia malengo ya kila mkakati na jinsi mikakati inavyohusiana na kusaidiana katika kutatua changamoto za upatikanaji, uwezo wa kununua na kumiliki vyandarua vyenye dawa kwa makundi yaliyo hatarini zaidi na malaria.*

## Hati Punguzo ya Wajawazito na Watoto

Hati Punguzo ya Wajawazito ilianzishwa mnamo Oktoba 2004 na Mpango wa Taifa wa Hati Punguzo. Lengo kuu la mkakati huu ni kukinga wajawazito na watoto wachanga na malaria kwa kuongeza upatikanaji wa vyandarua vyenye dawa kwa bei nafuu zaidi. Kwa kupitia mpango huu kila mjamzito ana haki ya kupata hati punguzo wakati anapohudhuria kliniki ya afya ya mama na mtoto. Hati hii ina thamani ya SH 3,250, na inaweza kutumiwa na wajawazito kununua chandarua chenye dawa kutoka kwa wafanyabiashara wanaoshiriki katika mpango huu.

Hati Punguzo ya Wajawazito ilikadiriwa kumkinga mjamzito pamoja na mtoto mchanga. Hata hivyo tafiti mbali mbali zilionyesha kuwa, kinamama wengi huacha kulala na watoto baada ya watoto hao kufikisha mwaka mmoja, hivyo basi watoto hawa hubaki hatarini na maambukizo ya malaria. Kutokana na sababu hii, Hati Punguzo ya Watoto ilianzishwa mwaka 2006 ili kukidhi mahitaji ya watoto kwa kusaidiana na Hati Punguzo ya Wajawazito. Lengo kuu la Hati Punguzo ya Watoto ni kuwapa kinga ya moja kwa moja watoto wachanga dhidi ya malaria kwa kuwaongezea upatikanaji wa vyandarua vyenye dawa.

Kwa kutipia mpango huu kila mtoto mwenye miezi 9 ana haki ya kupata Hati Punguzo wakati wa chanjo ya surua itakayomwezesha kununua chandarua chenye dawa kwa bei nafuu. Hadi kufikia mwezi Januari 2009, kadiri ya watoto laki 862,190 walikuwa wamejipatia vyandarua vyenye dawa kupitia Hati Punguzo ya Watoto.

Kutokana na ukweli kuwa vyandarua vyenye dawa ya kawaida hudumu kwa miaka miwili, kumekuwa na wasiwasi kuwa watoto walio na umri zaidi ya miaka miwili bado wako hatarini zaidi na maambukizi ya malaria. Hivyo basi kampeni hii ilianzishwa ili kukidhi mahitaji kwa kundi kubwa zaidi la watoto.

## Kampeni ya Usambazaji wa Vyandarua

Nchini Tanzania, ugonjwa wa malaria unachangia asilimia 43 ya mahudhurio ya watoto chini ya umri wa miaka mitano hospitalini, asilimia 35 ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano wanaolazwa, na asilimia 37 ya vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano. Katika juhudi zake za kupunguza vifo vitokanavyo na malaria na kuhakikisha idadi kubwa ya watoto chini ya miaka mitano wanapata kinga dhidi ya malaria, Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria kwa kushirikiana na wadau umeanzisha Kampeni ya Usambazaji wa Vyandarua kwa watoto chini ya miaka mitano. Kampeni hii inasaidiana na Mpango wa Hati Punguzo ya Wajawazito na Watoto kuwawezesha watoto kupata vyandarua vyenye dawa ya kudumu.

Kampeni hii ni fursa ya kipekee inayotolewa na Serikali ya Tanzania kusambaza zaidi ya vyandarua milioni saba bila malipo kwa watoto wote wenye umri chini ya miaka mitano kwa Tanzania Bara. Lengo kuu la kampeni ni kuongeza kwa kasi umiliki wa vyandarua na idadi ya wamiliki kwa kundi hili lililo hatarini kutoka asilimia 30 hadi asilimia 80 au zaidi.



*Waziri Mkuu, Mhe. Mizengo Pinda akitoa chandarua wakati wa kampeni ya majaribio wilayani Mpanda*

Kampeni hii inasaidiana na mpango wa Hati Punguzo ya Wajawazito na Watoto ili kuwawezesha watoto wenye umri wa zaidi ya miezi tisa kupata kinga dhidi ya malaria kupitia vyandarua vyenye dawa ya kudumu. Kampeni hii inaleta kwa mara ya kwanza teknolojia ya vyandarua vyenye dawa ya kudumu kwa muda mrefu zaidi hivyo kuyalinda makundi yaliyo hatarini kwa muda mrefu. Vilevile, kampeni hii inahusisha zoezi la uwekaji NGAO *iliyoboreshwa* kwenye vyandarua vya zamani. Zoezi hili linalenga kuongeza kinga kwa wanajamii wote kwa kuvipa vyandarua vyao nguvu dhidi ya mbu waenezao malaria kupitia uwekaji dawa.

Kampeni hii ilifanyiwa majaribio Septemba 2008 Wilayani Mpanda, uzinduzi wa kampeni ya majaribio ulifanywa na Waziri Mkuu, Mh. Mizengo Pinda. Hivi sasa kampeni hii inaendelea kutekelezwa nchi nzima. Kampeni hii itafuatiwa na Mkakati wa Keep-up unaolenga kutatua changamoto ya bei ya vyandarua vyenye dawa kwa kuwawezesha wajawazito na watoto kupata vyandarua vyenye dawa kwa bei ya SH 500/- tu kwa kutumia Hati Punguzo ya Wajawazito na Hati Punguzo ya Watoto.

## Mkakati wa Keep-Up

Mkakati huu unalenga kuendeleza matumizi ya vyandarua vyenye dawa ya kudumu kupitia mfumo wa Hati Punguzo. Mkakati unalenga kutatua changamoto ya bei ya vyandarua ambayo ilibainishwa kama kikwazo katika kumiliki vyandarua. Mkakati huu utaendeleza mpango wa sasa wa Hati Punguzo ya Wajawazito na Watoto kwa kupunguza bei ya nyongeza ya kununua vyandarua vyenye dawa ya kudumu hadi kufikia Tsh. 500/- tu kwa nchi nzima. Usambazaji wa Hati Punguzo hizi kwa wajawazito na watoto utafuata mfumo uliopo sasa kwa kupitia vituo vya afya ya mama na mtoto.

Mkakati huu utatekelezwa kuanzia katikati ya mwaka 2009 na utaendelea kwa miaka miwili ijayo. Mkakati huu utawapa wajawazito na watoto fursa kubwa zaidi ya kununua vyandarua vyenye dawa ya kudumu kwa bei nafuu zaidi ili kujikinga na malaria.

Mikakati yote, pamoja na kampeni zimepangwa na kutekelezwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kupitia Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na wadau. Mikakati hii inafadhiliwa kwa pamoja na Mfuko wa Fedha wa Dunia wa Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria, Benki ya Dunia na Mfuko wa Kupambana na Malaria wa Rais wa Marekani.

Vyandarua vyenye dawa ya kudumu vitapatikana kwa Sh. 500/- tu nchi nzima kupitia Mkakati wa Keep-up

## Balozi wa Malaria wa Afrika Ahudhuria Maadhimisho ...

*(Inatoka Uk. 1)*

Wakati wa maadhimisho, Bi. Chaka Chaka alitembelea kliniki za Afya ya Mama na Mtoto ili kujionea shughuli nzima ya utoaji wa Hati Punguzo kwa wajawazito na watoto ili kujikinga na malaria. Pamoja na hayo, balozi huyo aliweza kuonana na wadau wakuu wa malaria pamoja na viongozi wa mkoa na wilaya kwa ajili ya majadiliano ya hali ya malaria mkoani Mtwara na Tanzania kwa ujumla.

Wakati wa majadiliano, balozi wa malaria alishangwaza na idadi kubwa ya vifo vitokanavyo na malaria mkoani Mtwara. Hata hivyo, alikumbusha kuwa, licha ya kuwa serikali kuu na wahisani wanatekeleza mikakati mbalimbali ili kufikia malengo ya Abuja, viongozi wa serikali za mitaa na wanajamii wanahitaji kuwa mstari wa mbele kwenye kuhamasisha matumizi ya njia mbalimbali za kujikinga na malaria ikiwa ni pamoja na kutumia vyandarua vyenye dawa; na kuhamasisha na kuelimisha jamii kuondokana na fikra potofu na kujenga tabia ya kutafuta ushauri wa kitaalamu na tiba mara wanapohisi dalili za malaria.

Takwimu zinaonyesha kuwa, zaidi ya watoto 80,000 hufa kila mwaka kutokana na malaria, hivyo kufanya malaria kuwa ugonjwa unaosababisha vifo vingi zaidi nchini. Mtwara na Lindi ni mikoa iliyoathirika zaidi na ugonjwa wa malaria nchini Tanzania, ikifuatiwa na mikoa ya Kanda ya Ziwa ambayo ni pamoja na Kagera, Mwanza na Mara.

## Mganga Mkuu wa Mpanda Atudokeza Mafanikio ya Kampeni

*Wilaya ya Mpanda ilizindua kampeni ya taifa ya majaribio ya ugawaji wa vyandarua mnamo Septemba 2008. Zoezi hili la siku tatu lilihusisha ugawaji wa vyandarua na uwekaji dawa kwenye vyandarua vya zamani. Dk. Yahaya Husein, Mganga Mkuu wa Wilaya anatudokeza mafanikio katika utekelezaji wa kampeni hii.*

### Swali na Jibu

***Ukizingatia kuwa Mpanda ni Wilaya kubwa zaidi nchini Tanzania, Je mlijipanga vipi kutekeleza kampeni hii?***

Kabla ya kampeni tulikuwa na mwezi mmoja wa maandalizi, ambapo Halmashauri ya Wilaya ya kwa kushirikiana na Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malari na wadau tuliunda mpango kazi uliobainisha majukumu ya wahusika na kuelekeza utekelezaji. Vilevile ufuatiliaji wa mara kwa mara ulifanyika ili kuhakikisha kuwa watekelezaji wakuu wanatambua majukumu yao na changamoto zilizojitokeza zilitatuliwa katika ngazi ya Wilaya na Kitaifa. Mafunzo ya usajili, utiaji dawa, na ugawaji wa vyandarua na jinsi ya kutoa ripoti yalitolewa kwa Kamati za Afya za Mkoa na Halmashauri, Watendaji wa Kata na Vijiji na wanaojitolea. Vilevile watoto wote wenye umri wa chini ya miaka mitano walisajiliwa, shughuli zote hizi ziliambatana na uhamasishaji wa jamii.

***Changamoto Gani Ziliwakabili?***

Mpanda ni Wilaya kubwa zaidi Tanzania na wakazi wake wamesambaa katika sehemu mbalimbali, pia miundombinu na njia za mawasiliao ni duni; na hii ilifanya baadhi ya maeneo kuwa magumu sana kufikika, hivyo basi baadhi ya watoto walichelewa kusajiliwa.

Pia kutokana na kuhamahama kwa jamii za wafugaji, watoto katika jamii hizi walikosa kusajiliwa na wengine hawakuwepo wakati wa zoezi la ugawaji vyandarua. Katika Kata nyingine kampeni iliathiriwa na kutoeleweka kwa madhumuni ya kampeni na hii ilisababisha kusajiliwa kwa watoto wachache na kutolewa kwa vyandarua vichache kuliko ilivyopangwa.

***Je mmeweka mkakati gani wa kuwafikia watoto waliokosa vyandarua?***

Vyandarua vya ziada vilivyobaki kwenye Wilaya nyingine za mkoa wa Rukwa vitasambazwa kwa watoto waliokosa vyandarua Wilayani Mpanda. Kama idadi ya vyandarua hivyo haitakidhi mahitaji wa watoto hao, takwimu zao zitakusanywa na kuwasilishwa kwa Mganga Mkuu wa Wilaya kwa uratibu zaidi na Mpango wa Kudhibiti Malaria.

***Je una maoni gani kuhusu kampeni hii?***

Kampeni hii ni moja ya njia fanisi ya kuongeza upatikanaji wa vyandarua kwa kujikinga mbu waenezao malaria. Vilevile ushirikiano kati ya sekta mbalimbali unarahisisha utekelezaji wa zoezi kubwa kama hili, na husaidia huongeza ufanisi na hufikisha huduma katika muda mfupi zaidi.



*Watoto wilayani Mpanda wakitoka kupokea vyandarua vyenye dawa wakati wa kampeni ya majaribio*

## Mbinu za Kutatua Changamoto za Matumizi ya Vyandarua Vyenye Dawa

Katika miaka minne iliyopita Tanzania imeshuhudia uwekezaji mkubwa katika kufikisha zana za kujikinga na malaria kama vile vyandarua vyenye dawa katika jamii. Ingawa kumekuwa na mafanikio makubwa katika upatikanaji na bei nafuu wa vyandarua hivi, bado kuna changamoto katika matumizi ya vyandarua vyenye dawa. Changamoto hizi zinaonekana katika masuala mbalimbali yakiwemo ya miundo na rangi za vyandarua hadi imani za kimila na kidini ambazo hufananisha vyandarua na vitu kama sanda, mahandaki au makaburi. Ingawa changamoto hizi sio za kutisha, huathiri lakini kwa kiasi matumizi ya vyandarua katika Kaya. Hii inarudisha nyuma jitihada za kujikinga na malaria kwa kutotumia vyandarua ili kuepuka mbu waenezao ugonjwa huu.

Katika kukabiliana na changamoto hizi, Mradi wa Kuelimisha na Kubadili Tabia ya Jamii dhidi ya Malaria Tanzania (COMMIT) unatekeleza kampeni mahsus za mabadiliko ya tabia ambazo zinafikishwa kwa jamii husika kupitia majadiliano ya ana kwa ana ili kuzipatia jamii husika elimu na kuhamasisha matumizi ya vyandarua vyenye dawa kwenye jamii ambazo imani za kimila na kidimi zinaathiri matumizi hayo. Majadiliano haya hufanyika baina ya wakufunzi na mtu mmoja mmoja au vikundi, au kupitia warsha za vikundi vidogo vidogo katika jamii.

Kwa kupitia njia hizi ujumbe maalum unaolenga kubadilisha tabia kujadiliwa kwa pamoja na imani potofu hujadiliwa huku zikilinganishwa na ukweli, kupitia kutoa elimu kuhusu faida za kiafya na za kiuchumi za matumizi ya vyandarua. Mradi wa Kuelimisha na Kubadili Tabia ya Jamii dhidi ya Malaria Tanzania (COMMIT) una lengo la kuchangia juhudi za kupambana na malaria kwa kuhakikisha kuwa jamii za Kitanzania zinapata elimu ya kutosha kuhusu ugonjwa wa malaria na jinsi ya kutumia zana zilizopo ili kujikinga na ugonjwa huu.

Wadau wetu

Wahisani wetu

World Bank